

KINA CHA FIKIRA



KAULI YA WALIBORA

**"Ni amri ya
kukifanya
Kiswahili somo
la lazima katika
shule za msingi
na sekondari
ndiyo
imechangia
maenezi
mapana zaidi
ya Kiswahili
tangu enzi ya
Rais Moi."**

CHUO Kikuu cha Riara kilichoko kwenye barabara ya Mbagathi, Nairobi, kilipokea nakala zake za kwanza za gazeti la *Taifa Leo* wiki iliyopita. Nilibaini kwamba hakuna nakala ya gazeti hili la pekee la Kiswahili nchini Kenya iliyokuwa ikiletwa katika maktaba ya chuo. Maktaba ilinunua magazeti ya Kiingereza tu, si *Daily Nation*, si *Sunday Nation*, si *The Standard*, si *The Star*. Nilijuliza kwa nini chuo hiki kinakosa kabisa matoleo ya gazeti la pekee la Kiswahili nchini? Isitoshe, katika mauzo-iwapo sikosei—*Taifa Leo* ndilo gazeti la tatu kwa wingi wa nakala zinazouzwa kila siku nchini!

Magazeti ya Kiingereza ya kampuni ya usambazaji habari ya NMG niliyok-wishayataja yapo mbele, yakifuatwa na *The Standard* na kisha *Taifa Leo*.

Voyoyote iwayyo, gazeti la *Taifa Leo* linaandikwa na kuchapishwa kwa Kiswahili. Kiswahili ndiyo lugha ya tafifa ya Kenya, lugha rasmi (sambamba na Kiingereza) na lugha ya mawasiliano mapana au *lingua franca* kama wase-mavyo wataalamu. Unaweza kuongeza kwamba Kiswahili ndiyo lugha ya mawasiliano mapana katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAM) lugha rasmi tarajiwa (baada ya kupashishwa na bunge la Afrika Mashariki) na lugha ya utambulisho.

Ukweli ni kwamba hakuna lugha nyingine inayozungumzwa na wakazi wa Afrika Mashariki kama Kiswahili hata kama wapo wanaoii 'Chiswahili' kama baadhi ya Waganda na Wanyarwanda. Lakini mgogoro nilio nao una-husu nchi ya Kenya.

Je, haya madai makubwa makubwa ya kusema katika Katiba kwamba Kiswahili ni lugha ya taifa na lugha rasmi yana tija gani? Zamani zile za magazeti ya serikali *Kenya Times* na *Kenya Leo*, ofisi zote za umma zililazimika kununua nakala za magazeti haya. Kizazi cha sasa cha vijana huenda hakina habari kuhusu kuwepo kwa magazeti hayo mawili ya serikali ya KANU na ambayo sasa yamekufa na kuzikwa katika kaburi la sahau.

Ila ninapokumbuka amri ya kununu-



Kiswahili hakitapiga hatua bila mikakati, amri na mapinduzi

liwa kwa magazeti hayo na ofisi za umma, nakosa kujuliza kwa nini isi-we sheria kwamba gazeti la pekee la Kiswahili—lugha ya taifa, lugha rasmi, na lugha ya mawasiliano mapana-linunuliwe na kila asasi?

Naam, wapo watakaosema huo ni udikteta tena mbaya sana. Ila ukweli ni kwamba Kiswahili hakaendelea bila amri na mikakati ya mapambano na mapinduzi. Ni amri ya kukifanya Kiswahili somo la lazima katika shule za msingi na sekondari ndiyo imechangia maenezi mapana zaidi ya Kiswahili tangu enzi ya Rais Moi. Kwa sasa vipo vizazi vyta Wakanya waloliyamishwa kusoma Kiswahili kwa takriban miaka 14. Ni amri, ni udikteta na tazama tija ya kuwa na taifa la wasemajii wa Kiswahili.

Shukran muktubi wa Chuo Kikuu cha Riara kuitika wito wa mnyonge kama mimi.

hili somo la lazima katika shule za msingi na sekondari ndiyo imechangia maenezi mapana zaidi ya Kiswahili tangu enzi ya Rais Moi. Kwa sasa vipo vizazi vyta Wakanya waloliyamishwa kusoma Kiswahili kwa takriban miaka 14. Ni amri, ni udikteta na tazama tija ya kuwa na taifa la wasemajii wa Kiswahili.